Viashiria vya Ustawi
Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo (*)
Matokeo ya Utafiti wa CWIQ

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mwezi **Septemba 2006**, timu kutoka EDI zilifanya utafiti katika **Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo** Utafiti uliagizwa na kugharimiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kuwezeshwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya. Timu hizo zilitumia dodoso la CWIQ-Core Welfare Indicators Questionnaire katika kaya 450 zilizochaguliwa kwa nasibu katika wilaya hiyo. Ripoti kamili ya majibu inapatikana bure kwenye tovuti www.edi-africa.com/research/cwiq. Kipeperushi hiki ni muhtasari wa baadhi ya mambo muhimu.

SIFA BAINIFU ZA WAKAZI

Baada ya utangulizi katika sura ya kwanza, sura ya 2 ya ripoti inatoa majumuisho ya sifa bainifu za kaya na wakazi katika wilaya, ikiwa ni pamoja na ajira, kiwango cha elimu, hali ya ndoa ya mkuu wa kaya, yatima na malezi kwa watoto walio na umri chini ya miaka 18, uhusiano wa mwanakaya na mkuu wa kaya na idadi ya wanakaya. Baadhi ya takwimu muhimu zimeonyeshwa chini.

Sifa Bainifu za Wakazi kwa Ujumla

Wastani wa ukubwa wa kaya katika wilaya ni watu **4.9**.

Uwiano wa utegemezi wilayani ni wategemezi **1.2** (wenye umri chini ya miaka 15 au zaidi ya 60) kwa kila mtu mzima wa umri wa kufanya kazi (kati ya miaka 15 na 59).

12% ya kaya wakuu wake ni wanawake

Yatima na Malezi

1% ya watoto wenye umri chini ya miaka 18 wamepoteza wazazi wote wawili, **3%** wamepoteza baba pekee na **1%** wamepoteza mama pekee.

3% ya watoto wenye umri chini ya miaka 18 walikuwa hawaishi na baba wala mama, **8%** walikuwa wanaishi na mama pekee na **0.4** walikuwa wanaishi na baba pekee





ELIMU

Dodoso liliulizia kuhusu elimu kwa kila mwanakaya, ikiwa ni kujua kusoma na kuandika, mahudhurio shuleni, kutoridhika na huduma za shule na sababu zake, fursa katika shule za msingi na sekondari; umefanyika uchambuzi kijinsia, kiumri na kwa makundi ya kijamii na kiuchumi, kiwango cha umaskini, n.k. Sura ya 3 ya ripoti inafafanua taarifa hizi. Baadhi ya mambo muhimu yanaonyeshwa hapa chini.



● Watoto wenye umri wa shule ya msingi wanaoishi mwendo pungufu ya dakika 30 toka shule ya msingi ni **72%**, na kwa sekondari ni **14%**

● Kwa wanafunzi wote dodoso linauliza matatizo yanayowakabili. Kwa shule ya msingi wanaosema hakuna matatizo ni **66%**, na kwa sekondari ni **61%**. Grafu hapo chini inaonyesha sababu kuu za kutoridhika na shule.

KJU (Kiwango Jumla cha Uandikishwaji): Jumla ya watoto wa umri wa kwenda shule walio shuleni ikilinganishwa na jumla ya watoto wote wa umri wa kwenda shule.

KHU (Kiwango Halisi cha Uandikishwaji): Jumla ya watoto walio shuleni ikilinganishwa na jumla ya watoto wa umri wa kwenda shule.

Kusoma na Kuandika ni kwa mujibu wa wasailiwa





(*) Kazi ya utafiti, uchambuzi yakinifu na usambazaji wa taarifa za CWIQ imefanywa na Economic Development Initiatives (EDI), SLP 393, Bukoba - Kagera, Tanzania. http://www.edi-africa.com

Viashiria vya Ustawi
Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo (*)

AFYA

Sura ya 4 ya ripoti inahusika na taarifa juu ya viashiria afya vya msingi kama fursa za huduma ya afya, matumizi ya huduma za afya, kinga dhidi ya malaria, afya ya mama mjamzito, sababu za kutoridhika na huduma, viashiria lishe kwa watoto na mengine. Baadhi ya mambo muhimu yanaonyeshwa chini.

Waliohudumia katika Kuzaliwa Mtoto (kwa watoto chini ya umri wa miaka 5)



Viashiria vya Lishe (watoto wote chini ya umri wa miaka 5)

Watoto wafupi kwa umri wao (Utapiamlo wa muda mrefu)

Kudumaa	43%
Kudumaa sana	14%

Watoto wenye uzito mdogo kwa urefu wao (Utapiamlo wa muda mfupi)

Kuvia	1%
Kuvia sana	0%

KUDUMAA: mtoto kuwa mfupi akilinganishwa na umri wake. Hutokana na mtoto kuwa na utapiamlo wa muda mrefu.
KUVIA: mtoto kuwa na uzito mdogo akilinganishwa na urefu wake. Hutokana na mtoto kuwa na utapiamlo wa muda mfupi.

Viashiria vya Huduma za Afya



Sababu za Kutoridhika



Mahali Huduma ya Afya Ilikotolewa



Kinga Dhidi ya Malaria
38% ya kaya zimeripoti kutumia chandarua (angalao moja ya aina yoyote) kujikinga na malaria, na **47%** zimeripoti kutumia chandarua zilizotiwa dawa.

Fasili
Fursa ya Huduma ya Afya: Asilimia ya kaya zinazoishi mwendo chini ya dakika 30 toka kituo cha huduma ya afya.
Mahitaji: Asilimia ya watu walioripoti kuugua au kujeruhiwa katika kipindi cha wiki 4 kabla ya siku ya usaili.
Matumizi: Asilimia ya watu waliomwona mhudumu wa afya katika kipindi cha wiki 4 kabla ya siku ya usaili.
Kuridhika: Asilimia ya watumiaji walioripoti kutokuwa na matatizo na huduma za afya.

MIUNDOMBINU YA KAYA

Sura ya 7 ya ripoti ina taarifa za kina kuhusu miundombinu ya kaya kama vile vifaa vilivyotumika kutengenezea kuta, paa na sakafu; huduma muhimu za kaya kama aina ya chanzo cha maji ya kunywa, nishati inayotumika kwa kupikia na mwanga. Pia inahusisha umbali toka kwenye huduma muhimu kama barabara, shule, soko la chakula na usafiri wa umma.

Kaya zenye hati miliki au mkataba wa pango	2%
Kaya zilizopo mwendo pungufu ya dakika 30 toka chanzo cha maji ya kunywa	88%
Kaya zilizo na chanzo salama cha maji (bomba / kisima kirefu / pampu ya mkono / kisima kilichojengewa)	61%
Kaya zenye choo salama (kuflashi kwenye mfereji wa maji taka/tangi au shimo lililofunikwa)	80%
Kaya zenye mfumo bora wa ukusanyaji taka	15%
Kaya zitumiazo mafuta ya taa kama nishati kuu kwa kupata mwanga	82%
Kaya zitumiazo kuni kama nishati kuu ya kupikia	95%
Kaya zenye nyumba ambazo sakafu zake ni za saruji au vigae	5%
Kaya zenye nyumba ambazo kuta zake ni za matofali ya kuchoma /saruji / zege	33%
Kaya zenye nyumba ambazo kuta zake ni za tope / matofali ya udongo	67%
Kaya zenye nyumba ambazo paa zake zimeezekwa kwa mabati	35%

Umilikaji wa Vyombo vya Mawasiliano

Ingawa asilimia ya kaya zinazomiliki simu za mezani na runinga katika wilaya hii ni ndogo sana kiasi cha kutohesabika, **5%** ya kaya zinamiliki simu za mkononi na **53%** ya kaya zinamiliki redio.

Viashiria vya Ustawi
Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo (*)

AJIRA

Ripoti pia ina sura yenye taarifa za kina kuhusu ajira kwa wanakaya wenye umri kuanzia miaka 5, katika siku 7 zilizopita na kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita. Utafiti ulijumuisha hali ya ajira, shughuli kuu, aina ya mwajiri, ajira isiyo toshelevu, ukosefu wa ajira na huduma za kaya.

Sekta ya Ajira



Aina ya Mwajiri

59% ya watu wanaajiriwa na mwajiri binafsi, **39%** wanaajiriwa na kaya, na **2%** wanaajiriwa na serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali au waajiri wengine.

Ajira ya Watoto

51% ya watoto wa umri kati ya miaka 5 na 14 hufanya kazi. Kati yao, **88%** hufanya kazi za kaya na **3%** hufanya kazi za kilimo

Asilimia ya Watoto Wanaofanya Kazi za Nyumbani

(kwa watoto wenye umri kati ya miaka 5 na 14)



Ajira Isiyo Toshelevu

(wafanyakazi ambao wamekuwa wakifanya juhudi za dhati kutafuta njia za kujiongezea kipato)



UTAWALA

Mojawapo ya mambo mapya katika ripoti ni sura kuhusu utawala. Ripoti ina taarifa kuhusu mahudhurio katika mikutano, kuridhishwa na viongozi na sababu za kutoridhika. Pia inaarifu juu ya asilimia ya kaya zinazopata taarifa za mapato na matumizi ya fedha za umma, na inadadisi sababu za kutoridhika na ngazi mbalimbali za serikali.

Walioripoti Kuridhika na Utendaji wa Viongozi katika Ngazi ya...



Fedha za Umma



Sababu za Kutoridhika na Viongozi

(Pamoja na waliojibu 'sijui')



Viashiria vya Ustawi
Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo (*)

USTAWI

Ripoti ina taarifa juu ya viashiria ustawi, ikiwa ni pamoja na shida katika kutosheleza mahitaji kadhaa muhimu ya kaya, umilikaji wa mifugo, ardhi na raslimali, mtazamo juu ya hali ya uchumi wa kaya na jumuiya, pamoja na hali ya usalama katika jumuiya. Pia inataarifu kuhusu mabadiliko ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Baadhi ya mambo muhimu yanaonyeshwa hapa chini.

Mabadiliko
(ikilinganishwa na mwaka mmoja kabla ya utafiti)

Hali ya Kiuchumi
52% ya kaya zinaripoti kuwa hali ya kiuchumi ya kaya imeshuka, na **24%** zinaripoti imepanda.

45% ya kaya zinaripoti kuwa hali ya kiuchumi ya jumuiya yao imeshuka, na **24**% zinaripoti imepanda.

Hali ya Uhalifu na Usalama
20% ya kaya zinaripoti kuwa hali ya uhalifu na usalama imekuwa mbaya zaidi, wakati **50%** zinaripoti kuwa ni bora zaidi.

Umilikaji wa Mifugo Wakubwa (ng'ombe, punda, n.k.)
2% ya kaya zinaripoti kuwa zinamiliki ng'ombe wachache zaidi, na **3**% kuwa zinamiliki ng'ombe wengi zaidi ya mwaka uliotangulia utafiti.

Ugumu katika Kutosheleza Huduma za Afya
16% ya kaya ziliripoti kuwa na matatizo ya mara kwa mara au mara zote katika kutosheleza mahitaji ya huduma za afya.

Umilikaji Ardhi
Wastani wa kumiliki ardhi uliripotiwa kuwa ekari **3.4** kwa kaya.

Ugumu katika Kutosheleza Mahitaji ya Chakula



Umilikaji wa Raslimali

Vyombo vya Usafiri
1% ya kaya zinamiliki gari au lori, **37%** zinamiliki baiskeli na asilimia ya kaya zinazomiliki pikipiki ni ndogo sana kiasi cha kutohesabika.

Raslimali nyingine
0.4 ya kaya zinamiliki toroli na **3%** zinamiliki cherehani.

Pembejeo za Kilimo
10% ya kaya zinaripoti kutumia pembejeo za kilimo. Kati ya hizo, **80%** ya kaya hutumia mbolea ya chumvichumvi, **21%** hutumia mbegu zilizoboreshwa, **15%** hutumia dawa za kuulia wadudu, na asilimia ya kaya zinazotumia samaki wadogo wa kufuga, ndoano na nyavu za uvuvi au pembejeo nyingine za kilimo ni ndogo sana kiasi cha kutohesabika.

TASWIRA YA WILAYA

Ikilinganishwa na Wilaya 28 za CWIQ pamoja na Malengo ya MKUKUTA ifikapo mwaka 2010

	Kibondo	Wilaya 28 za CWIQ*
Uwiano wa utegemezi	1.2	1.0
Wastani wa idadi ya wanakaya	4.9	4.9
Kaya zenye wakuu wa kaya wanawake	12%	19%
Wakuu wa kaya wenye wake wengi	23%	12%
Watoto waliofiwa na wazazi wote wawili	1%	2%
Watoto waliofiwa na baba pekee	3%	7%
Watoto waliofiwa na mama pekee	1%	2%
Watoto wasioishi na wazazi wao	3%	29%
Watoto wanaoishi na mama pekee	8%	13%
Watoto wanaoishi na baba pekee	0%	4%
Wanafunzi wasioridhika na shule zao (na sababu)	34%	47%
Ukosefu wa vitabu	31%	41%
Ufundishaji duni	7%	17%
Upungufu wa walimu	77%	55%
Miundombinu mibovu	13%	37%
Msongamano	13%	19%
Watoto wanaoishi mwendo pungufu ya dakika 30 toka shule ya msingi	72%	69%
Kaya zilizo mwendo pungufu ya dakika 30 toka kituo cha huduma ya afya	62%	41%

	Kibondo	Wilaya 28 za CWIQ*
Watumiaji walioridhika na huduma za afya	88%	77%
Kaya zinazomiliki simu za mkononi	5%	19%
Kiwango cha upungufu wa ajira	19%	22%
Waliojiajiri katika kilimo	54%	39%
Kaya zinazotumia pembejeo za ziada za kilimo	10%	33%
Wastani wa mifugo wakubwa (ng'ombe, punda, n.k) kwa kaya	0.2	3.7
Wastani wa kumiliki ardhi kwa kaya (ekari)	3.4	4.5
Kaya zenye hatimiliki ya makazi	2%	9%
Kaya zilizo mwendo chini ya dakika 30 toka chanzo cha maji	88%	84%
Kaya zinazotumia vyandarua kujikinga na malaria	38%	30%
Kaya zinazoripoti kuwa na shida kulipia huduma za afya mara kwa mara / mara zote mwaka uliopita	16%	23%
Walioridhika na uongozi wa kitongoji (wilaya za vijijini tu)	91%	87%
Walioridhika na uongozi wa kijiji/mtaa	87%	80%
Walioridhika na uongozi wa kata	84%	72%
Walioridhika na uongozi wa wilaya	82%	64%
Walioridhika na diwani	81%	66%
Kaya zinazoripoti kuwa hali ya kiuchumi ya kaya zao imeshuka katika mwaka uliopita	52%	51%
Kaya zinazoripoti kuwa hali ya uhalifu na usalama imekuwa mbaya zaidi	20%	21%

* **Wilaya 28 za CWIQ** ni wastani wa wilaya 28 zilizochaguliwa kufanyiwa utafiti wa CWIQ wa mwaka 2006/2007: Wilaya za Bariadi, Bukoba (V), Bukombe, Bunda, Chamwino, Hanang, Kahama, Karagwe, Kasulu, Kibondo, Kigoma, Kishapu, Korogwe, Maswa, Meatu, Mpwapwa, Muheza, Musoma, Ngara, Ngorongoro, Rufiji, Singida, Kilosa, Morogoro na Manispaa za Tanga, Dodoma, Shinyanga na Temeke.

Ulinganisho na Wilaya 28 za CWIQ pamoja na Malengo ya MKUKUTA